

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



S. L.P 1055, ARUSHA  
Simu : (027) 2503538/ 2507928  
Nukushi: (027) 2505973  
Barua pepe: [rbcarusha@pccb.go.tz](mailto:rbcarusha@pccb.go.tz)  
Wavuti : [www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**JUNI 1, 2020**

**WATATU WAFIKISHWA MAHAKAMANI KWA KUKUTWA NA SHEHENA  
YA BIDHAA BANDIA ZA KILIMO NA MIFUGO ZENYE THAMANI YA  
ZAIDI YA SHILINGI MILLION 200**

TAKUKURU Mkoani Arusha, inatarajia kuwafikisha mahakamani **Anselm Anthony Kessy, Mary Anselm Kessy** na **Godwin Anselm Kessy** ambao ni wamiliki wa kampuni ya **ANICROP Services Ltd.** ya Jijini Arusha inayojishughulisha na uuzaji wa pembejeo za kilimo na mifugo ndani na nje ya mkoa wa Arusha.

Wamiliki hao wa kampuni ya ANICROP, wanatuhumiwa kutengeneza bidhaa baandia na kubadili tarehe ya bidhaa zilizoisha muda wa matumizi na baadae kuzuiza kwa watumiaji katika maeneo mbalimbali nchini, jambo ambalo ni kinyume cha sheria ya Chakula na Madawa Sura ya 219 na sheria ya Ulinzi wa Mimea Sura ya 133.

Awali, Taarifa ya kutendeka kwa makosa hayo zilipokelewa mnamo mwezi Januari 2020 ambapo uchunguzi ulianzishwa katika eneo la biashara na katika maghala yanayomilikiwa na kampuni hiyo yaliyopo kijiji cha Ikiurei kata ya Kirany halmashauri ya wilaya ya Arusha.

Uchunguzi huu ambao uliratibiwa na TAKUKURU mkoa wa Arusha, ulihusisha taasisi kadhaa za serikali zikiwemo; Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TMDA),

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu (TPRI) na Wataalam wa kilimo na mifugo kutoka ofisi ya mkuu wa mkoa wa Arusha.

Uchunguzi huu ulibaini uwepo wa shehena kubwa ya bidhaa za kilimo na mifugo zilizoisha muda wa matumizi yenye thamani ya zaidi ya **shilingi million mia mbili na tatu, laki tano na kumi na tano elfu (Tzs. 203,515,000/-)**, kiasi kikubwa cha vifungashia vya aina mbalimbali ambavyo bado havijatumika na mashine za kufungasha bidhaa, vinavyoashiria uwepo wa kiwanda bandia cha kuzalisha bidhaa hizo.

Uchunguzi wa tuhuma hizi umekamilika na kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka, Watuhumiwa wanatarajiwa kufikishwa mahakamani leo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha kwa makosa saba (7) yakiwemo makosa ya Sheria ya Chakula na Madawa (Food, Drugs and Cosmetics Act Sura ya 219) na sheria ya Ulinzi wa Mimea (Plant protection Act, Sura ya 133).

#### **Ufafanuzi wa Makosa:**

TAKUKURU mkoani Arusha, ilipokea taarifa mnamo tarehe 20.01.2020 kutoka kwa Msiri ikieleza kwamba, kampuni ya ANICROP SERVICES LTD ya Jijini Arusha inayojishughulisha na uuzaji na usambazaji wa madawa ya kilimo na mifugo inakiuka sheria, kanuni na taratibu za mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMD), TRA pamoja na TPRI katika kuendesha shughuli zake.

Taarifa hiyo iliendelea kueleza kwamba, kampuni hiyo inamiliki maghala ambayo hayajasajiliwa na TMDA na inauza bidhaa zilizoisha muda wa matumizi kwa kuzijaza upya bidhaa hizo katika vifungashio vipya na kuandika tarehe mpya ya muda wa kuisha matumizi huku tayari bidhaa hizo zikiwa zimeisha muda wa matumizi.

Pia ilielezwa kwamba kampuni hiyo inashirikiana na kampuni moja ya Kichina iitwayo Farm Lord kutengeneza bidhaa bandia na kuonesha kwamba bidhaa hizo zimetoka Ufaransa.

Aidha mtoa taarifa huyo aliendelea kueleza kwamba, mamlaka za serikali zinazohusika na kodi na usimamizi wa bidhaa za kilimo na mifugo zimekuwa zikifanya ukaguzi wa mara kwa mara katika kampuni hiyo lakini hakuna hatua zozote zinazochukuliwa, hivyo kuashiria uwepo wa vitendo vya rushwa.

TAKUKURU Mkoa wa Arusha inaendelea kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Arusha kwa ushirikiano wanaotoa kwa taasisi kwa kutoa taarifa za wanaojihusisha na vitendo vya rushwa kwenye taasisi za serikali na maeneo mengine. Hii inaashiria mwamko chanya wa wananchi katika kushiriki mapambano dhidi ya Rushwa.

TAKUKURU inawahamasisha wananchi kuendelea kutoa taarifa hasa katika kipindi hiki tunachoelekea kwenye maandalizi ya uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani na kuwahakikishia kuwa taarifa zitakazopokelewa zitafanyiwa kazi kwa haraka.

Aidha TAKUKURU Mkoa wa Arusha inatumia fursa hii kuwaonya wale wote wanaojiandaa kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu ujao, kutokutoa rushwa kwa lengo la kutengeneza mazingira ya kukubalika au kuanza kampeni kabla ya muda, kwani iwapo watabainika watakamatwa na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

**Imetolewa na:**

**SABAS SALEHE,**

**KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M) ARUSHA**

**JUNI 1, 2020**

---